



**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA**



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA KWA UMMA

**UFAFANUZI KUHUSU TAARIFA ZA UBALOZI WA MAREKANI
KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA AGOSTI 12 MWAKA 2018**

Leo 15 Agosti 2018 Ubalozi wa Marekani Tanzania kupitia tovuti yake [_tz.usembassy.gov_](http://tz.usembassy.gov) umetoa taarifa inayotoa tuhuma dhidi ya Serikali, Tume na Jeshi la Polisi. Tume inatoa ufafanuzi na rai kama ifuatavyo:

1. Tume inautaka Ubalozi huo uthibitishwe wanachokieleza juu ya uchaguzi mdogo wa Jimbo la Buyungu na kata 36.
2. Uchaguzi Mdogo huwa hauna waangalizi wa Kimataifa, je Ubalozi huo umetoa wapi taarifa hizo? Na hayo waliyoyaona, wameyaona kwa kutumia utaratibu upi na sheria ipi?
3. Katika Jimbo la Buyungu mgombea wa Ubunge mmoja wapo kupitia (Chadema) alijitokeza kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii na kueleza hisia zake na kusema bayana kuwa amekubaliana na matokeo, na ameshukuru kwa kuwa Uchaguzi huo umemjenga.
4. Kilichotokea Arusha ni vurugu mitaani mbali na maeneo ya vituo vya kupigia kura. Kwa kuwa vurugu hizo zilipelekea jinai kufanyika vyombo husika vinashughulikia.

5. Hakuna chama chochote cha siasa kilichoshiriki Uchaguzi huo, kilichojitokeza kusema na kuthibitisha kuwa uchaguzi haukuwa huru na haki.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuufahamisha umma kuwa Tanzania ni nchi huru na inaendesha chaguzi zake kwa mujibu wa Katiba yake na Sheria za Uchaguzi.

Tume inasisitiza kwamba uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Buyungu na kata 36 wa tarehe 12 Agosti mwaka 2018, umefanyika kwa uhuru na haki kuanzia mchakato wamaandalizi hadi siku ya kupiga kura yenyewe. Aidha ambaye hajaridhika bado Sheria za Nchi zinampa fursa ya kuwasilisha malalamiko yake kwenye mamlaka mbalimbali zilizopo.

Imetolewa leo tarehe 15 Agosti, 2018.

**CHRISTINA NJOVU
AFISA HABARI MWANDAMIZI**